**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0739958638**
**Mkuu wa Shule 0767 958638**
**Makamu M/s 0752449481**
**Patron 0767863867**

**SHULE YA SEKONDARI ILULA**
**S.L.P 29,**
**MAZOMBE - IRINGA.**
**12 JUNE 2023**
**Namba ya Shule NECTA: S.0515**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ILULA, HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO MKOA WA IRINGA MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………..…

Shule ya Sekondari ilula ipo umbali wa Kilometa 45 upande wa Mashariki mwa Mji mkuu wa Mkoa wa Iringa, Pembeni mwa barabara ya Iringa - Morogoro. Usafiri wa basi kutoka mjini Iringa unapatikana katika kituo cha mabasi Stand kuu Iringa, Nauli ni Shilingi 2000 tu, Shuka kituo kidogo cha basi cha Ilula - Isele.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14.08.2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13.08.2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.08.2023**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili (2) za rangi nyeusi zenye malinda mawili kila upande, suruali isiwe ya kubana (modo) chini na juu.
ii. Mashati mawili (2) rangi nyeupe tetron ya mikono mirefu.
iii. Sare ya Michezo ni bukta nyeusi, raba jozi moja na track suit ya bluu (inaweza kuvaliwa wakati wa baridi)
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
vii. Sweta darkblue mshono shingoni "V"
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali mbili za kaki zenye malinda mawili kila upande.
ix. Tai mbili nyeusi ( ndefu)
x. Tisheti ya blue (form six), Nguo ya kazi.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari ya kutosha (counter Book 10)
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
iv. Godoro 01 (6 ft x 2½ ft)
v. Mashuka Jozi 2 (pink), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*blue);*
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Vifaa vingine aje na jembe moja lenye mpini pamoja na ufagio mmoja (hard bloom)

**2.3 MICHANGO YA SHULE (ILIPWE NMB TAWI LOLOTE, AKAUNTI NAMBA 62301200028 SHULE YA SEKONDARI ILULA)**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII,**

**............................................................**

**SHADRACK PETER MBILINYI**
**MKUU WA SHULE.**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0767958638**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752449481**
- **Mwandamizi Taaluma 0769687605**
- **Mwandamizi Malezi 0762453525**

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

**KILOLO DISTRICT COUNCIL**

**ILULA SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

*(To be completed by Medical officer in respect to all FORM FIVE)*

Pupil's full name…………………………………………………………………

Age…………………………..Year……………………..Sex……………………

Blood count (Red and white)…………………………………………………….

Stool Examination………………………………………………………………..

Syphilis and other venereal Diseases Test……………………………………

…………………………………………………………………………………..……

TB test ………………………………………………………………..………….

Eye Test………………………………………………………………………….

Ears…………………………………………………………………..…………

Spleen……………………………………………………………………..……

Abdomen ……………………………………………………………..……

Urine for Protein Test……………………………………………………………

Test for Pregnancy (for girls only)……………………………………………

**Additional information** (if any) e.g. physical defects, impairment,
Infections, chronic or family diseases e.t.c

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….…………

I certify that the above is fit /unfit to pursue his/her lessons/duties as required.

Station …………………………………… Signature………………………..…….

Date ……………………………………… Designation……………………………

**Note: Medical Officer.**

At the time of examination please treat the individual for anything you note for pupils/employee. This completed form should be sent to the school with your acceptance form brought when you come to school. No pupils/person/employee can be enrolled /employed without certification on

**SHULE YA SEKONDARI ILULA**

**ORODHA YA VITABU VYA MUHIMU KWA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO**

**GENERAL STUDIES**

- UNDERSTANDING ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES – J. B. RWAMUNGU & SOSPETER .M. DEOGRATIAS
- CONTEMPORAL APPROACH FOR ADVANCED LEVELGENERAL STUDIES NOTES – NYAMBARI .M. NYANGWINE

**GEOGRAPHY**

- PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCE LEVEL –JAMES E. KINUNDA
- ESSENTIAL PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCE LEVEL - JOSEPH NJIKU
- PHYSICAL GEOGRAPHY – BARNET
- INTERGRATED APPROACH – DAVID WAUGH

**ENGLISH LANGUAGE**.

- OXFORD ADVANCED LEARNER'S DICTIONARY
- ADVANCE LEVEL ENGLISH LANGUAGE 1 FORM 5&6 – SHEDRACK NDAMBO &JAMES KINUNDA
- RECOMMENDED ENGLISH LANGUAGE ONE HANDBOOK FOR ADVANCE LEVEL – PASCHAL SALAWI
- THE REAL ENGLISH TEXTBOOK FOR ADVANCE LEVEL FORM 5 – DR. KIDEGE MICHAEL

**KISWAHILI**

- KAMUSI YA KISWAHILI (**TUKI**)
- **VITABU VYA MASHAIRI** –CHUNGU TAMU, - FUNGATE LA UHURU, - KIMBUNGA.
- **VITABU VYA RIWAYA** – VUTA N'KUVUTE, - MFADHILI.
- **VITABU VYA TAMTHILIYA** – KIVULI KINAISHI, - MORANI.
- KISWAHILI 1 KIDATO CHA TANO NA SITA.

**HISTORY**

- ESSENTIALS IN ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER 1 & 2 BY SALEH YASSIN
- CONTEMPORARY HISTORICAL EVENTS VOLUME I & II BY SHIBITALI C.K. TUMAINI

- GENERAL HISTORY OF AFRICA BY ASSA OKOT